# Amini Kutoka Moyoni

[Ndugu Branham anasoma Yakobo 5:12 kanda inapoanza—Mh.]

> . . .*wala kwa kiapo kinginecho chote: bali ndiyo yenu na iwe ndiyo; na siyo yenu iwe siyo; msije mkaanguka katika hukumu.*
>
> *Kuna mtu wa kwenu aliyepatikana na mabaya? na aombe. Ana moyo wa kuchangamka? na aimbe zaburi.*
>
> *Je, kuna yeyote mgonjwa kati yenu? na awaite wazee wa kanisa; nao wamwombee, na kumpaka mafuta kwa jina la Bwana:*
>
> *Na kuomba kwa imani kutamwokoa mgonjwa huyo, na Bwana atamwinua; na ikiwa amefanya dhambi, atasamehewa.*
>
> *Ungameni dhambi zenu ninyi kwa ninyi, na kuombeana, ili mpate kuponywa.* Maana *kuomba kwake mwenye haki kwafaa sana akiomba kwa bidii.*
>
> Eliya *alikuwa mwanadamu mwenye tabia kama sisi, akaomba kwa bidii mvua isinyeshe*: *na mvua haikunyesha juu ya nchi muda wa miaka mitatu na miezi sita.*
>
> *Akaomba tena,* mbingu *zikatoa mvua, nayo nchi ikazaa matunda yake.*
>
> *Ndugu zangu, ikiwa mmoja wenu amepotea kutoka kwenye kweli, na mtu mwingine* akamrejeza*;*
>
> *Ajue ya kuwa yeye amrejezaye mwenye dhambi hata atoke katika upotevu wa njia* yake, *ataokoa nafsi na mauti, na itaficha wingi wa* dhambi.

2 Katika mlango wa mwisho wa Kitabu cha Marko, mlango wa 16, na kifungu cha mwisho cha mlango wa 16 wa Marko Mtakatifu, tunasoma Maneno haya:

> Baadaye, *akaonekana na wale kumi na mmoja walipokuwa wakila, akawakemea kwa kutokuamini kwao na ugumu wa mioyo yao, kwa sababu hawakuamini*. . .yeye aliyefufuka kutoka kwa wafu.
>
> *Akawaambia, Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe.*
>
> *Aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini, atahukumiwa.*
>
> *Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; Katika jina langu watatoa pepo; watanena kwa lugha mpya;*

*Watashika nyoka; hata wakinywa kitu cha kufisha, hakitawadhuru kabisa; Wataweka mikono juu ya wagonjwa, nao watapata afya.*

3 “Kuomba kwa imani kutamwokoa mgonjwa huyo.” Sasa, tunapoinamisha vichwa vyetu katika maombi, hebu sote, pamoja, katika njia yetu, na kila mtu katika njia yake, tuwaombee maombi ya imani hawa wagonjwa asubuhi ya leo. Kisha ninataka kuwawekea mikono, pamoja na wazee. Ndipo tumefanya kile hasa Neno la Mungu lililosema. Maana, hapo ndipo ninapoenda moja kwa moja, katika Ujumbe wangu.

Sasa na tuombe.

4 Baba yetu wa Mbinguni, tunapokuletea wimbo huu, sauti ya *Amini Tu,* unakuonyesha hisia zetu kuhusu Neno Lako. Na kama vile wagonjwa wametiwa mafuta kulingana na Neno Lako, na sasa tutaomba maombi haya ya imani, kadiri tujuavyo, kutii amri Zako. Nasi tunatambua, hata katika udhaifu wetu, Wewe unaweza hata na zaidi kushinda udhaifu wetu kwa Nguvu na wema Wako. Na kisha tutawaleta wazee huku, kuweka mikono juu ya wagonjwa, tukitimiza kila agizo tunalojua ambalo limetolewa na Bwana wetu.

5 Nasi tunaomba, Bwana, kwamba tumepata neema machoni Pako, baada ya miaka hii yote, bado tunajaribu kutii amri Yako. Na sasa naomba, pamoja na kundi hili dogo asubuhi ya leo, kama vile ulivyotutuma, kwa kuwa ni wahitaji, watu hawa ambao wako hapa kuombewa. Nasi tunafanya maombi haya kwa kila mmoja wao. Unaijua mioyo yao na unajua shauku zao.

6 Nami naomba maombi haya ya imani, pamoja na kanisa hili, kwamba utawadhihirishia kila shauku waliyo nayo. Na iwe halisi sasa hivi. Na jalia, wanapoondoka kwenye kanisa hili, leo, na waende kama Ibrahimu wa kale, wakiziita dalili hizo kana kwamba hazikuwapo, na kukataa chochote ambacho kingekuwa kinyume na baraka ambayo tumeomba. Umeahidi katika Neno Lako ya kwamba itatimia, nasi tunaamini.

7 Sasa, pamoja na watu hawa ambao umewachagua na kuwaita wawe wahudumu na wazee, tutaweka mikono juu yao kana kwamba. . .kana kwamba tulikuwa tunawabatiza. Nao wametiwa mafuta. Maombi ya imani yametolewa, na mikono inawekwa juu yao. Tunaomba kwamba imani yao sasa itakutazama Wewe, Ee Mungu Mwenyezi, na waponywe. Katika Jina la Yesu tunaomba.

8 Sasa, ninawaomba wazee, waje moja kwa moja hapa kwenye mstari, tunapowawekea mikono. Na wakati kila mmoja unapoweka mkono wako kwenye. . .[Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

9 . . .mtanipa usikivu wenu mkamilifu, kwa dakika chache tu, tafadhali. Ninajaribu kutochukua muda mwingi sana, ninapoweka saa yangu ya mkono hapa, nipate kuwa na hakika.

10 Na, Ndugu Beeler, nafikiri uko kwenye kinasa sauti, upande huo mwingine. Na Leo na Gene hawapo hapa. Kwa hiyo nataka wewe, tafadhali, kurekodi ushuhuda huu ambao nitatoa katika dakika chache, ukatumiwe Ndugu Boze, alichukue jambo hili.

11 Ningependa kusoma, asubuhi ya leo, kutoka kwenye—kwenye Kitabu cha Marko Mtakatifu, mlango wa 12. Tunataka kuchukua sehemu ya hili na kulisoma, na kwa sababu ni Neno takatifu la Mungu, lisiloghoshiwa. Nasi tunaamini ya kwamba Mungu yuko katika Neno Lake. Je, mnaamini hivyo? Nasi tunaomba ya kwamba Mungu ataongeza baraka Zake Kwake, tunapolisoma, nami nina hakika ya kwamba ataongeza.

12 Kisha ninataka kuchukua sehemu nyingine ya Neno Lake, kutoka katika Matendo, mlango wa kwanza. Nasi tutasoma kutoka hapo. Nami ninamwomba Bwana kama ataongeza baraka Zake kwenye—kwenye kusomwa kwa Neno Lake.

13 Nilikuwa naangalia tu hapa. Nilikuwa na alama hapa kwenye Biblia ya—yangu, ambayo nilitaka kusoma kutoka kwake, kwanza, lakini sidhani kama ninaweza kuipata kwa wakati huu. Samahani tu kidogo, mpaka niweze kuipata, nikiweza. Nilidhani nilikuwa nayo.

> . . . Yesu *akawaambia, Mwaminini Mungu.*
>
> *Kwa maana, amin, nawaambia, Ukiuambia mlima huu,* Ng'oka . . .; *wala usiwe na shaka moyoni* mwako, *bali . . . uamini kwamba mambo hayo* unayosema *yatatokea; yatakuwa yako* uliyosema.

14 Sasa, katika Matendo, m—mlango wa kwanza na kifungu cha 8.

> *Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu: nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, na katika . . . Uyahudi, na Samaria, na hata* miisho *ya nchi.*

15 Ningependa kuvuta usikivu wenu kwa Neno la Bwana, asubuhi ya leo, kwa muda mfupi tu. Nami ninawatakeni mlizingatie sana. Sikilizeni kwa makini. Thamani ya Neno hili!

16 Baada ya miaka ishirini na mitano ya huduma kwa ajili ya Bwana, katika kazi Yake na katika Neno Lake; na baada ya huu kuwa, kuingia katika mwaka wangu wa kumi na mbili wa uinjilisti wa kimataifa; na kwa neema ya Mungu, kukutana na makumi ya maelfu ya—ya watu; na kumwona Bwana wetu katika kampeni zetu wenyewe, akiwavuta, sasa kama nilivyoona, Kwake, loo, moja kwa moja kuelekea watu milioni mbili, ama milioni moja na laki tano, kitu kama hicho, mikutanoni. Nimefikia hitimisho hili, na katika juhudi zetu zote, na kadhalika. Haiwezekani kwa Mungu kuwafanyia watu lolote mpaka wawe wameamua kwanza kama ni Kweli au la. Kamwe huwezi. Haidhuru . . .

17 Nimeona wajuzi wakubwa sana wa Bwana wetu, ka—katika Neno, ambao wangeweza kueleza Neno vizuri zaidi kuliko mtu yeyote niliyepata kumwona, na hata hivyo wasingeweza kufanikisha mpango.

18 Nami ninamwazia, asubuhi ya leo, mtu fulani ambaye nafikiri ana mojawapo ya vipindi bora zaidi vya redio hewani. Lakini kuna, kwa namna fulani, mtu huyo hawezi kukiendeleza kipindi chake tena. Huyo ni Dk. Wyatt, mwalimu halisi. Lakini kuna kasoro; sijui ilipo. Analo ono, analo wazo, ana uwezo, lakini kamwe hawezi kuundeleza huo mpango, kwa namna fulani. Mpango huo alio nao upo juu ya Neno kabisa, nao unapaswa kuufanya ulimwengu utubu.

19 Nami niliona hapa, si muda mrefu uliopita, huko Louisville, nilipomwona Dr. Mordecai Ham na wanatheolojia wengi wakuu ninaowajua, ambaye ni mhubiri bora sana kuliko vijana wa miaka thelathini na minane au arobaini, mwinjilisti mwenye nywele nyekundu alienda jukwaani, akawapita watu hao, nao wakaketi nyuma. Na kusimama pale usiku ule, hakuwa na sehemu moja kwa kumi au sehemu moja kwa mia ya yule mhubiri ambaye wale watu walikuwa wameketi nyuma yake, ingawa alikuwa na mpango wa Mungu na kuuweka kwa: Billy Graham.

20 Nimeona mambo hayo. Na katika kuyaona, basi ninafikia hitimisho hili. Haidhuru wewe ni nini, Mungu hana budi kuliandaa kusanyiko. Na haijalishi kama ningeweza kusimama hapa asubuhi ya leo na kuwafufua wafu, na kuwarejesha vilema kwenye hali yao ya kawaida, na, hata hivyo, Mungu hayuko katika mpango huo, haungeenda popote. Mungu hana budi kuwa katika huo mpango.

21 Na mtu yeyote, anajulikana, tabia yake inajulikana kwa matendo yake. Haijalishi yeye ni nani, matendo yake yanathibitisha tabia yake. Kama ukimchukua mtu, haijalishi anajaribu kuwa mzuri kiasi gani, ikiwa matendo yake ni maovu, wema wake wote utakuwa ni bure. Na neno la mtu ni tabia yake. Mtu ambaye neno lake halifai kitu, basi hutawahi kumwamini mtu huyo, kwa sababu neno lake halifai kitu.

22 Kwa hiyo, basi, Mungu, Baba yetu, tabia Yake na matendo Yake yanathibitisha kile alicho. Sasa, tunajua ya kwamba ulimwengu huu ulikuja hapa kwa Muumba fulani mkuu. Usingeweza kutokea tu.

23 Sasa, ninataka dakika hizi chache tu ziwe rahisi iwezekanavyo. Bali ninawatakeni muliingize ndani, nikiomba ya kwamba Roho Mtakatifu ataliingiza moja kwa moja kwenye nuru inayofaa.

24 Sasa, kama ungetazama tu na kuona miti ikikua; na matawi na majani, jinsi yanavyokuja na kuondoka, na maua; msimu wa kuchipusha majani, msimu wa kupukutika majani, majira ya baridi kali, majira ya kiangazi. Inabidi kitu Fulani kiwe nyuma

ya hayo. Hakuwezi kuwa na mti isipokuwa kuwe na akili ya kuufanya mti. Haidhuru ni maisha ya namna gani yangekuwa ndani yake, hapana budi kuweko, nyuma ya hiyo, akili fulani ya kuufanya jinsi ulivyo.

25 Sasa wazia hilo, moja kwa moja sasa. Usiache likupite. Liwazie, kwa kilindi. Kwa maana, ukiona somo letu la Maandiko, Yesu alisema, "Kama utasema moyoni mwako!"

26 Si katika akili zako; haitafanya kazi humo kamwe. Haijalishi ni kiasi gani utajaribu kuifanya itende kazi, haitafanya kazi, kwa sababu ni ya kiakili na ina mwisho.

27 Lakini wakati kitu chochote ni cha Milele, hakina mwisho, wala hakina mwanzo. Chochote chenye mwisho, mwanzo, kina mwisho. Lakini ni mambo yale tu ambayo hayana mwanzo. Na Mungu pekee ndiye hana mwanzo wala mwisho. Na, halafu, kuwa na mambo haya yaliyo na mwanzo, ilibidi kuwe na kitu kisicho na mwanzo, kuanzisha mwanzo.

28 Mti wa kwanza uliopata kuumbwa, ambao, kama ule ambao Yesu aliulaani hapa, kasema, "Tunda lolote lisikue kutoka kwako tangu sasa, mtu asile kutoka kwako," ilibidi kuwepo, mahali fulani, mti huo ilibidi uwe na mwanzo. Na ulikuwa na mwisho, wakati Maneno ambayo, kutoka midomoni mwa Yule aliyeupa mwanzo, yaliupeleka hadi mwisho. Kwa hiyo, mnaona jinsi Maneno Yake yalivyo ya Milele.

29 Lakini tumelikubali Neno tu kwa msingi wa kiakili. Na tumeona mapungufu mengi kabisa, hata yamewafikisha watu mahali ambapo ni vigumu sana kujua la kuamini. Wana ninii tu, wana miisho mingi iliyolegea kwa—kwa dini yao. Wanakimbilia kwenye matawi *huku*, na matawi *huko*, yanayofikia mwisho, na hawa hapa wanarudi wakitambaa. Huduma kubwa zinaanza nao wanakimbia kama Wamethodisti, Wabaptisti, na Wapentekoste, na wote hawa. Na, muda si muda mwajua, wanapata wazo dogo la kiakili, ndipo wanakimbilia kwenye hilo tawi nao wanafurahi sana. Lakini, muda si muda mnajua, wanajikuta mwisho.

30 Lakini vitu pekee vinavyodumu, ni vitu vya Milele, navyo vitu vya Milele ni Mungu.

31 Sasa, ukiangalia, mtu hujulikana kwa ninii yake. . .tabia yake inajulikana kwa matendo yake. Kama tungewazia jinsi Mungu anavyoonyesha tabia Yake kwa matendo Yake. Ana tabia Yake Mwenyewe, Naye alifanya kazi Zake. Na ukiangalia kazi Zake, jinsi zilivyo kuu!

32 Sasa hebu nimpe changamoto kila mwanasayansi duniani anijengee mti mmoja. Hebu nimpe changamoto kila mwanasayansi ulimwenguni anifanyie kitawi kidogo cha unyasi. Na haiwezekani kabisa.

33 Vema, inaonekana kama, basi, juu ya kuyatafakari mambo hayo, ya kwamba kunaweza kuwa na kuwekwa, kwa kusoma

Neno, imani ambayo ingepita dhana za kiakili, kuingia moyoni. Yesu alisema, "Kama utasema moyoni mwako!"

34 Sasa, sote tunafadhaika katika akili zetu, na tunatoka na kusema, "Loo, niliona *hilo* likifanywa. Naam. Mimi. . ." Na mara moja moja, kuchupa, kupiga hatua, na kadhalika, lakini inaonekana kana kwamba haiwezi kuendelea sawasawa. Ni kwa sababu tunajaribu kuchanganya ya kiakili na ya kimbinguni. Hayana uhusiano moja na nyingine, hata kidogo. Wasomi watasema jambo moja, na wa kimbinguni watasema lingine.

35 Na mtu yeyote anayeongozwa na Roho wa Mungu hachukui wazo lolote la kiakili, lakini anaongozwa na Roho wa Mungu kutoka moyoni mwake. Haeleweki. Watu wanasema, "Loo, inawezekanaje?"

36 Hivi sasa ninapokea barua na simu, "Unamaanisha, Ndugu Branham, ya kwamba hutaenda kwenye nchi za ng'ambo? Baada ya ninii hizi zote kuu. . ."

37 Lakini, inaonekana nzuri sana, lakini Kitu fulani ndani kabisa, kilisema, "Kuwa mwangalifu."

38 Na, kwa hiyo, hatuangalii tunayoona. Tunaangalia vile vitu ambavyo hatuvioni, lakini, kile ambacho Mungu anasema moyoni. Na kama tungeweza kuzingatia mambo hayo, ni zaidi sana vipi kwa uponyaji wa Kiungu. Kama Mungu alitoa ahadi, nayo inatia nanga moyoni, vema, tunahitaji wasomi wa nini tena? Siangalii mateso yangu. Siangalii dalili zangu. Ninaangalia kile Mungu alichosema juu yake. Kwa sababu, hata hivyo, Yeye ndiye Bosi, na Bosi mkuu. Kama daktari alisema *hivi na hivi*. . .

39 Sasa, ukijaribu kuhadaa hilo, halitafanya kazi. Ukijaribu kulihoji moyoni mwako, useme, "Ndiyo, Neno la Mungu ni la kweli. Ninaliamini Hilo. Naamini litatimia. Nafikiri *hivyo*." Sasa, kama hiyo ni kiakili, afadhali hata uache kuliwazia.

40 Mpaka kitu Fulani kishuke ndani yako, kinachosema tu ndivyo, wala hamna lingine. Hakuna pepo wa kutosha kutoka matesoni wanaoweza kamwe kuitikisa kutoka kwako. Ni kitu Fulani kilicho ndani, kinachoitwa "moyo." Hapo ndipo imani ya kweli hupata mahali pake pa kutulia.

41 Wasomi watajaribu kutoa hoja juu yake. "Sasa na tuwe na busara tu." Lakini imani haina hoja. Ina kitu kimoja tu, na, hicho ni, Neno la Mungu ni la kweli. Loo, hapo ndipo nafsi huweka miguu yake, na kutulia Milele papo hapo, kwa maana Mungu alisema hivyo. Si kuhadaa, lakini kujua.

42 Na dunia, ikiwa ni kazi ya Mungu, inazungumza kabisa na kushuhudia Utu Wake. Hapana budi kuwe na Mungu, la sivyo kusingekuwa na dunia. Hapana budi kuwe na Muumba, la sivyo kusingekuwa na uumbaji. Na kama Neno hili, aliloiumba dunia

nalo, likitoa ahadi, halina budi kuumba yale hasa dunia hii iliumba, kwa Neno Lake, hapo mwanzo.

43 Mungu aliposema, "Na iwe," na huenda ilichukua miaka bilioni kumi. Sijui ilichukua muda gani. Lakini kwamba ilichukua muda gani, hiyo haikuwa na maana yoyote, kwa maana Mungu ni wa Milele. Naye alisema, "Na iwe," nayo ikaanza kusitawi, kwa maana Mungu alichukua Neno Lake Mwenyewe na kuliamini.

44 Na kama Neno Lake la uumbaji Wake, kazi Yake hapa, inathibitisha kwamba Yeye ni Muumba, basi kwa nini hatuwezi kuchukua Neno Lake kwa yale linayosema na kuliamini? Kwa sababu, ni Neno lile lile la Muumba. Sasa, kazi Zake zinashuhudia.

45 Na, sasa, kabla Mungu, Yule asiyekosea, hajaweza kunena lolote, halina budi kuwa kamilifu. Kwa sababu, linaweza tu—linaweza tu. . .Kama linatoka kwa Mungu, linatoka kwa njia kamilifu.

46 Sasa angalieni hili. Watu wote, kila kitu, watu wanajulikana kwa matendo yao.

47 Wakati lile Daraja kuu la Manispaa lilipojengwa huko Sydney, Australia, walipoagizia kote ulimwenguni na kupata wajenzi wa madaraja, wasanifu majengo, na kutoka . . . walitaka kuvuka rasi hu—huko Sydney, Australia, kwenda Sydney Kusini, wasanifu majengo na wote wakaja, wakachimba udongo na kuupima. Na wote wakafikia hitimisho hili, "Haiwezekani." Kasema, "Ghuba nzima imejaa mchanga mwepesi. Nao udongo hautashikamana vya kutosha. Utahama mahali mahali. Kwa hiyo, ikiwa daraja lingejengwa, ingekuwa ni hatari kujaribu kupita juu yake."

48 Basi hatimaye kulikuwa na mtu ambaye alikuwa mtu wa maono, mjenzi wa madaraja huko Uingereza. Akaja huko. Naye akauangalia huo mchanga. A—akauchunguza. Akapima udongo. Akapima maji kwa bildi. Aliyaangalia yote, kwanza.

49 Loo, ninapenda hilo. Akayaangalia yote, kwanza. Yesu alisema, "Mtu akinunua shamba, au akienda kukabiliana na jeshi, kwanza huketi chini na kuhesabu gharama." Kila mmoja wenu hapa madhabahuni asubuhi ya leo, mngeketi pale kwenye viti vyenu kabla ya kuja kutiwa mafuta, na kutafakari maana yake, haingekuwa tu ni kupitia mstari wa maombi, bila mpangilio, ingekuwa ni kwenda kule kwa ujasiri thabiti, ya kwamba, Mungu alikuwa ameliahidi na Mungu aliweza kulitimiza Neno Lake.

50 Kwa hiyo, mtu huyu akapima udongo. Akapima. . .kila sehemu mle ndani iliyokuwa na mchanga mwepesi. Na, hatimaye, akaenda kwa viongozi. Akasema, "Nitajenga hili daraja, na litakuwa salama."

51 Wajenzi wa madaraja wa Marekani na sehemu mbalimbali za ulimwengu walicheka tu na kusema, “Huyu mtu ni kichaa. Hakuna mtu anayeweza kuweka daraja kuvuka hapo.” Kasema, “Hata kuku angetembea kwenye daraja ambalo lingejengwa, lingezama. Daraja halingeweza kustahimili. Mitetemo ya hata mbwa akikimbia kuvuka daraja, ambayo italitetemesha daraja,” kasema, “ingeutikisa mchanga, nalo daraja lingeporomoka. Haiwezekani.”

52 Lakini mtu huyu alikuwa ni mtu wa ono, naye alijua alichokuwa anazungumzia, kwa maana kitu fulani ndani yake kilimwambia angeweza kufanya hivyo.

Mungu, tupe wanaume kanisani, namna hiyo!

53 Sasa, kutokana na utafiti wote wa kisayansi, ambao, haingewezakana, sayansi ilithibitisha ya kwamba isingewezekana. Lakini mtu huyu alikuwa na ono angeweza kulijenga, kwa hiyo akachukua kandarasi hiyo.

54 Haraka akaingia kazini. Akaanza kupima udongo. Akaanza kupima, na kupima kwa bildi vilindi vya sehemu yenye mchanga mwepesi. Akajaribu kila bolti. Akajaribu kila kipande cha—cha mbao, kila kipande cha chuma, kila zege. Kila kitu ilibidi kujaribiwa kikamilifu. Kwa sababu, ji—jina lake mashuhuri, na sifa yake na uwezo wake, vilitegemea kama daraja hilo lilisimama au la.

55 Na kama mtu wa dunia hii, kwa ono, angekuwa na uhakika kwamba kila kitu kilijaribiwa kikamilifu kabla ya kukiweka kwenye daraja, kwa sababu ya sifa yake na kwa sababu ya jina lake, ni zaidi sana vipi Baba yetu wa Mbinguni aliyebarikiwa alijaribu kila Neno ambalo liliwahi kusemwa au kuandikwa katika Biblia. Alijaribu kila Neno, kila nabii. “Na kila mwana amjiaye Mungu hana budi kujaribiwa.” Nyenzo zinazoingia katika Barabara hii kuu, kila jiwe, kila nyenzo, kabla ya kuwekwa kwenye—kwenye Mwili wa Kristo, haina budi kujaribiwa, kurudiwa. “Kila mwana amjiaye Mungu hana budi kujaribiwa kwanza.” Hakuna ubaguzi; kila mmoja! Kila nabii, kabla hajaweza kuandika katika Biblia hiyo, alijaribiwa na Roho Mtakatifu.

56 Kama vile tu yeye, huyo mjenzi wa daraja, samahani, nimesahau jina lake, nililijua, siku kadhaa zilizopita nilikuwa nikisoma makala hiyo, jinsi alivyopima kila kitu. Alitafuta makanika bora sana aliyeweza kupata. Akamchukua mtu bora sana wa zege. Alipata walio bora zaidi ambao angeweza kupata, kuweka pamoja kilicho bora kuliko vyote alivyokuwa navyo.

57 Loo, nafsi yangu ingelia “haleluya” kwa Mungu, ninapowazia ya kwamba Mungu huweka katika Kanisa Lake walio bora kuliko wote awezao kupata. Mungu huwachukua watoto Wake na kuwajaribu kwa majaribu yaliyo magumu sana, kisha anawaweka katika Mwili wa Kristo kwa sababu

wamejaribiwa. Wanaamini. Wamepitia majaribu. Wamekuwa na uzoefu. Wao ni mashahidi Wake. Wanajua wanachozungumzia. Sio tu dhana ya kiakili, bali wamezaliwa mara ya pili, kwa Roho Mtakatifu wa thamani, na kujaribiwa kwa wakati na kurudiwa, mpaka roho zao zimewekwa kama jiwe gumu sana kuelekea Kalvari. Naam, wamejaribiwa na wakati. Wao ni mashahidi wa Uweza Wake. Na kwa njia hiyo, Mungu anajenga daraja kutoka duniani hadi Utukufuni, ili msafiri apate kuja kwenye njia kuu, aketi chini ya mti, wakati wa kupunga kwa jua, kwa nyenzo zilizojaribiwa na wakati, wale wanaoliamini Neno la Mungu. Haijalishi kuna dalili gani, hali ya mambo, hiyo haitazuia. Mungu ana nyenzo zilizojaribiwa na wakati kama shahidi, Naye anaziweka.

58 Basi mjenzi huyu mashuhuri wa daraja, wakati hatimaye . . . Wasanifu mijengo walisimama kando kando, wakamwambia huyo mjenzi, wengi wa hao wakosoaji, "Halitasimama kamwe."

59 Ndivyo ambavyo wamesema, "Kanisa halitainuka kamwe." Ndivyo ambavyo wamesema, "Siku za miujiza zimepita." Ndivyo ambavyo wamesema, kwamba, "Dini ya mtindo wa kale haiwezi kufurahiwa tena."

60 Lakini, loo, mtu huyu alipoweka nyenzo hizo zote pamoja, alichimba. Akachukua mashine za kupulizia, na akapulizia sehemu hizo za mchanga mwepesi. Aliingia chini, chini, chini, kwa mamia ya futi chini ya maji, mpaka akaupeperushia mbali ule mchanga mwepesi, mpaka akaiweka zege imara kwenye mwamba chini ya bahari. Loo, ilikuwa ni gharama, naam.

61 Na chochote kinachostahili kuwa nacho, kina gharama inayoambatana nacho. Jinsi wokovu huu ulivyo mkuu! Gharama kuu jinsi gani!

Lakini, hatimaye akafika chini ya mchanga mwepesi.

62 Naye Mungu amewachukua Wakristo na kuwajaribu, na kuwajaribu, ilimbidi kuwapiga burashi, na kuwapiga burashi, na kuwapiga burashi, mpaka hatimaye, moja ya siku hizi, Yeye atashuka kwenye Mwamba imara. Mtu fulani huchukua tu tukio hili duni la kupeana mikono na kujiunga na kanisa, na kunyunyiziwa mara chache, ama kubatizwa ama chochote kile, Naye anaosha mchanga wote mwepesi tena mpaka atakapotia nanga kwenye ule Mwamba, Kristo Yesu. Pepo wote walio katika mateso hawawezi kumtikisa.

63 Mjenzi huyo wa daraja alijua alichokuwa akifanya. Basi wakati, hatimaye, baadhi yao walisema, "Halitasimama. Litakuwa hatari kwa chochote kupitia."

64 Aliwaleta, karibu, kundi la wahandisi, pamoja na garimoshi. Na siku hiyo walipopita kutoka Sydney Kusini, wakienda Sydney Kaskazini, kuvuka, aliweka yapata treni nane kubwa za mizigo zilizojaa kabisa. Naye akamweka meya wa jiji kwenye gari, kisha akaingia mbele yake, akitembea, amebeba bendera.

Na wakati lile jeshi kubwa na treni nane kubwa zilizojaa mizigo, zikivuka daraja hilo, huku yule mjenzi akiongoza, akitangulia, hata halikutikisika.

65 Naye Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, ambaye Ndiye Mbunifu wa Kanisa, alikuja katika dunia hii na kuweka msingi. Alipokutana na ibilisi, alijaribiwa kwa Neno la Mungu, Naye akasema, "Imeandikwa, 'Mtu hataishi kwa mkate pekee.'" Alipompeleka mpaka kinara cha hekalu, alisema, "Imeandikwa." Mnaona nyenzo alizokuwa akiweka katika Kanisa Lake? Akampeleka mlimani, na kumwonyesha miradi yote mikuu ambayo angeweza kuwa nayo; akasema, "Imeandikwa."

66 Neno lote la Mungu lilijaribiwa na wakati. Naye ndiye Kapteni mkuu anayetutangulia, huku koti Lake Mwenyewe lenye damu likipepea, kwamba, kwa upendo wa ukombozi wa Damu ya Yesu Kristo, amenunua Kanisa, kwa Roho Mtakatifu aliyejaribu kila bolti na kila mtu ambaye amewahi kutia nanga katika Kanisa hili kuu la Mungu aliye hai. Nyenzo zilizojaribiwa na wakati ndizo hufanya hivyo.

67 Naye anaposonga mbele, utawala mkuu ukija nyuma Yake, kama Kanisa lililozaliwa mara ya pili la Mungu aliye hai, Yeye hasogei, kwa sababu tumepokea Ufalme ambao hauwezi kutikiswa. Umechimbwa mpaka kwenye Mwamba imara, wa Kristo Yesu, akiwa ndiye Jiwe Kuu la Pembeni. Na anapotutangulia, akiwa na koti Lake Mwenyewe lililolowa damu, akiandaa njia, ni ishara ya ukombozi.

68 Mashahidi! "Mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, na Uyahudi, na Samaria." Kanisa Lake linasimama kama shahidi Wake. Sasa, asubuhi ya leo, ningetaka kusema hili na kuwaachieni hili. Sisi ni mashahidi Wake baada ya kumpokea Roho Mtakatifu. Kwa maana kunaweza kuwa na jambo moja tu unaloweza kushuhudia, hilo ni, kile unachojua kuwa ni Kweli.

69 Jamaa huyo angeweza kushuhudia, baada ya kupeperusha mchanga wote na kuufikia mwamba imara kwenye kifua cha dunia. Alikuwa shahidi kwamba huo ungeweza kushikilia. Aliweka Kipima mionzi na mitambo kwenye vipande hivyo vikubwa vya nyenzo na akajaribu kila kimoja. Alikuwa shahidi kwamba zingeweza kushikilia, kwa maana aliona zikitoa nguvu zake na ikashikilia.

70 Na sisi ambao tumezaliwa mara ya pili kwa Roho Mtakatifu, ambao tumejazwa na Nguvu za Mungu, ambao tumeonja Uzima wa Milele wa Mungu, naye Huyo anaishi ndani yetu, ni mashahidi wa wema Wake, na Neno Lake, na Nguvu Zake. Sio kukisia tena. Ni kujua-hivyo, kwa tukio.

71 Nuhu, alipojenga safina, alitoa ushahidi kwa ulimwengu usio na uadilifu kwamba kulikuwa na Mungu mwadilifu. Ingawa ilionekana kuwa wazimu wakati ilipokuwa inajengwa, lakini

ilithibitika kuwa ndiyo mashua pekee ambayo ingeelea kupitia dhoruba. Na ilipokuwa inajengwa, ilikuwa. . .Aliuhukumu ulimwengu usio wa haki, na kuwahesabia haki wale walioiamini.

72 Ni dhihaka jinsi gani, wakati mwingine, Mungu afanyavyo mambo, machoni pa mwanadamu. Je, uliwahi kusimama kuwazia ni mbao za aina gani ambazo Nuhu alitumia kujenga mashua hiyo? Ilijengwa kwa mbao za mshita. Na hizo ndizo mbao laini sana zinazoweza kupatikana. Ni kama tu balsamu. Ni. . .Mbona, ukiutupa ziwani kule nje, ungezama katika dakika tano. Ni mti wa balsamu, au mshita, una mashimo ndani yake. Na je, si ajabu kwamba safina iliyopaswa kustahimili yale majaribu ya maangamizi makuu yaliyotangulia gharika, ilitengenezwa kwa mbao laini? Naam, ilikuwa inatumika.

73 Na wakati fulani tunapokuwa wagumu sana na wasiopindika katika njia zetu, Mungu hawezi kututumia kwa lolote.

74 Lakini hii ndiyo sababu Yake ya kufanya hivyo: Je, mliona? Baada ya kuitengeneza, basi alichemsha lami, au utomvu fulani, ulikuwa, kutoka kwa miti mingine. Sasa, hii ina maana gani? Alipoweka safina pamoja, ilitengenezwa kwa mti huu mwepesi, laini. Ungeweza kuubeba kote, rahisi sana, ni mwepesi sana na wenye kupindika kwa urahisi. Na kisha akakata mti mwingine ambao ulikuwa msonobari. Nao wakautwanga huo, jinsi walivyokuwa wakiipata, kuutwanga na kuutwanga, mpaka wakatoa utomvu kwake. Halafu akachukua utomvu huu na kuumimina ndani ya mbao hizi nyepesi, na mashimo madogomadogo yaliyokuwa kwenye hizo mbao nyepesi yakajazwa na huo utomvu, yakafunikwa, yakaufanya mgumu kuliko chuma.

75 Naye Mungu alilitwaa Kanisa Lake, ambao wanajifanya tupu wenyewe, wala si kitu ila wanaoweza kupindika mikononi mwa Mungu. Mungu alimkata Mwanawe Mwenyewe, na kuuondoa Uhai kutoka kwa Mwanawe, kwa kupigwa na kuchubuliwa, na kuumwaga ndani ya mwaminio; naye anahifadhiwa, tayari kwa hukumu. Hicho ndicho kitu pekee kitakachostahimili hukumu.

76 Ilipitia moja kwa moja juu ya hukumu, maana ilipitia moja kwa moja. . .Yale maji yalikuwa ndiyo hukumu, na ikapita hukumuni. Ilikuwa ni ushahidi kwamba Mungu alijua alichokuwa akifanya. Nuhu alifuata Neno la Mungu. Mambo mengi yangeweza kusemwa.

77 Danieli alikuwa shahidi ya kwamba kulikuwa na Malaika Mbinguni, ama Mungu Mbinguni, ambaye alijua siri za moyo, kwa maana alimtuma Malaika Wake na kumwokoa Danieli. Wengine wengi walikuwa mashahidi.

78 Yesu alipokufa msalabani, mbingu zilitoa ushuhuda. "Hizo hapo nyenzo. Jambo ndilo hilo." Kama mtaona, viumbe vyote vinaishuhudia.

79 "Moja kwa moja katikati ya mchana." Mungu alipokuwa ametabiri, hapo awali, wakati Sabato ingekoma, alisema, "Itakuwa wakati ambapo jua litatua mchana." "Na tangu saa sita hadi saa tisa, kulikuwa na giza." Ilikuwa ni nini? Jua... Sasa, giza halimaanishi kuwa lina nuru kidogo ndani yake. Giza ni giza tupu kabisa, giza sana, kama ilivyokuwa huko Misri, mpaka liliweza kuguswa. Hakuna mwale wa mwanga!

80 Nalo jua likashuhudia, "Huyo hapo. Hizo ndizo nyenzo ambazo Mungu atajengea Kanisa." Mwezi na nyota zilitoa ushahidi. Alipokufa, mbingu zilishuhudia. Nchi ikateuka, miamba ikapasuka. Dunia ikatoa ushahidi. Nao watakatifu waliolala katika nchi, mavumbi ya nchi, wakainuka, wakatoa ushahidi.

81 Watu huko Pentekoste, walipokuwa wanafanya mzaha, Petro alisimama na kutoa ushahidi kwa baadhi ya Uhai huo uliopigwa ukatolewa Kwake pale Kalvari, ukamiminwa ndani ya Petro, katika umbo la Roho Mtakatifu. Naye akasimama hapo kama shahidi, Neno la Mungu, ndipo akashuhudia kwa andiko kutoka katika Maandiko, yaliyosema, "Enyi watu wa Uyahudi, nanyi mkaao Yerusalemu, jambo hili na lijulikane kwenu, na msikilize maneno yangu. Kwa maana hawa hawajalewa kama mnavyodhani, bali neno hili ndilo lililonenwa na nabii Yoeli, 'Itakuwa katika siku za mwisho, nitaimwaga Roho Yangu juu ya wote wenye mwili.'" Alikuwa shahidi.

82 Sasa tunaingia katika siku hizi za mwisho na za uovu, wakati Yeye atakuwa na mashahidi. Hana budi kuwa na mashahidi. Mungu yu hai. Neno la Mungu ni la Milele.

83 Sasa hebu turudi kwenye usomaji wetu wa Maandiko. Yesu, akishuka kutoka mlimani, alikuwa na njaa. Naye akatazama mtini, wala hapakuwa na tunda juu yake. Yeye, pengine, hakuinua sauti Yake.

84 Hakuwahi kusimama, kasema, "Sasa waungwana, simameni upande mmoja. Ninataka kuwaonyesha uweza Wangu." Akasema... "Nami nina uwezo wa kuufanya mti huo kufanya hivi na hivi." Kamwe hakusema hivyo.

85 Alimwendea tu. Hakupata ki—kitu chochote juu yake, kwa hivyo akasema, "Hakuna mtu atakayekula kutoka kwako," akaondoka.

86 Petro akasikia. Na kesho yake, alipopitia hapo, loo, ule mti ulikuwa ungali pale, bali ulikuwa umekufa. Naye akatoa tamshi juu yake, jinsi mti ule ulivyokauka upesi, kutoka kwenye mizizi yake. Yesu akasema, "Hapana..."

87 Na, angalia, halikuwa ni kosa la huo mti. Wakati wa tini ulikuwa bado. Bali alifanya hivyo ili kujitukuza Mwenyewe, kujithibitisha Mwenyewe. Kwa. . . Yeye alikuwa ni Masihi, na huo ulikuwa ni mmoja wa shuhuda kwamba Yeye alikuwa ni Masihi. Huo ulikuwa ni muhuri wa Umasihi Wake. Muhuri wa mwisho ulikuwa ni ufufuo Wake, kupaa Kwake. Huo ulikuwa ni muhuri wa mwisho wa Umasihi Wake. Alichofanya kilikuwa ni thibitisho ya kwamba Yeye alikuwa hivyo. Sasa, Yeye kamwe hakwenda huku na huku, akasema, "Miti yote na ife." Alifanya hivyo tu pale ili kwamba wale wanafunzi, ambao walikuwa waandike Maandiko haya baadaye, waweze kujua ya kwamba Yeye alikuwa ni Masihi. Mnaona?

88 Sasa, basi, Petro alipouliza swali hili, "Tazama, jinsi mti unavyonyauka upesi!"

89 Ndipo akawaambia, "Ukiuambia mlima huu, 'Ng'oka, ukatupwe baharini,' wala usiwe na shaka, bali uamini ya kwamba yale unayosema yatatimia, yatakuwa yako."

90 Sasa sikilizeni. Hiyo ni sehemu ya nyenzo katika uchumi huu mkuu wa Mungu, merikebu hii kuu tuliyomo, merikebu ya kale ya Sayuni, katika Mwili wa Kristo.

91 Sasa kwa ushuhuda! Imekuwa muda, nimetazama hili. Na sasa sikilizeni kwa makini sasa kwa mafundisho kidogo.

92 Kumekuwa na nyakati maishani wakati wote. . . wakati nimeyaangalia mateso, na kuona wale waliokuwa wanaumizwa na kuteswa kwa nguvu za pepo, moyo wangu unawalilia tu. Na, hata hivyo, wamenipigia simu, na katika mikutano, kelele hizo, na kuhama, na kuteka, na kuvuta, na ni vigumu sana kusema "hapana" kwa watu hao. Kusema kweli, siwezi kufanya hivyo; mtu husema kwa ajili yangu. Siwezi kuwafikia. Jinsi moyo wangu unavyowalilia. Siku baada ya siku mimi hupitia mateso ya hilo, na huwa nashangaa wakati mwingine.

93 Na, mimi, basi najifariji, kwa kurudi kwenye Maandiko, na kumwona Yeye akipitia mahali pale pa Bethesda, na kuwaona hao vilema wote na wanaoteseka; akamwendea mtu mmoja, akamponya, akiwa amelala juu ya godoro, akaondoka na kuwaacha wengine. Lakini, bado, chini moyoni mwangu, hilo hunifanya. . . haliuondoi mwasho huo. Loo, jinsi ninavyotamani kungekuwa na jambo ambalo lingeweza kutokea!

94 Ndipo nimeona, kule Portland, Oregon, wakati yule mwendawazimu usiku ule alipokimbilia jukwaani, kuniua. Ninakumbuka pale, jambo fulani lilitokea, na halikuwa la kiakili hata kidogo. Kiakili, ningetoroka kama wahubiri wengine walivyofanya. Lakini, sikukimbia. Kulikuwa na kitu; Mungu alikuwa anajitayarisha kuonyesha nguvu Zake.

95 Wakati mmoja, alisema, "Tulieni na mjue ya kuwa mimi ni Mungu." Kama Kanisa lingesimama tu kimya kwa muda wa kutosha! Mungu atafanya jambo fulani dogo, nao wote

watachangamka na kukimbia huku na huku, wakilifanya, mnaona, wanatoka nje ya mapenzi ya Mungu. Tulieni.

96 Wakati mmoja alikuwa anaenda kuonyesha Nguvu Zake katika Bahari ya Shamu. Alisema, "Bahari ya Shamu, wewe tulia tu." Naye akawapitisha watoto Wake moja kwa moja katika hiyo. Vipi kama wangegeuka, waseme, "Hebu tulifanye tena, Bwana"? Isingetokea. Bila shaka isingetokea.

97 Wakati mmoja alihitaji muda kidogo wa kupiga vita. Mungu alilisimamisha tu jua, kule, kutazama kile atakachofanya. Naam. "Sasa, jua, simama tu kimya, huko, kwa dakika chache. Nitakuonyesha kitu." Sasa vipi kama, kesho yake, Yoshua aseme, "Jua, simama kimya"? Isingetukia. Mungu alikuwa akitaka kufanya jambo fulani. Alikuwa anataka kutoa ushahidi kwa Nguvu Zake. Neno Lake, Yeye ni Mwenyezi, Naye amelitolea ushuhuda.

98 Wakati mmoja, kulikuwa na kipofu aliyetoka Yeriko. Basi Yesu alipokuwa akipita, yule kipofu akapiga kelele, "Nihurumie!" Nayo Biblia ilisema, "Naye Yesu akasimama kimya, akasema, 'Mleteni hapa.'" Loo, jamani! Kristo akasimama kimya, kwa maana Mungu alikuwa anaenda kumtumia kuonyesha Nguvu Zake.

99 Huenda kulikuwa na vipofu mia moja zaidi barabarani; sijui. Labda kuhani akisema, "Njoo hapa kidogo! Wewe ni Nani uliyewafufua wafu? Wafufue. . . Tuna makaburi yaliyojaa wao. Tulisikia ulimfufua Lazaro." Lakini, Mungu alikuwa akithibitisha Umasihi Wake. Hilo ndilo alilokuwa akifanya. Bila shaka.

100 Sasa, mara nyingi nimekuwa nikishangaa kinachotendeka. Lakini kuna mahali ambapo wanadamu wanaweza kuishi, karibu sana, katika Uwepo wa Mungu, si kwa kuchagua kwako, ni kwa uteuzi wa Mungu, kwamba unaishi mahali hapo, ambapo usomi wako hauna uhusiano wowote nalo.

101 Huko Afrika Kusini, nilipewa changamoto na kundi la wachawi. Nami nikiwa nimesimama pale, mmoja kati ya dazeni au zaidi, nao wakijaribu kuniroga. Lakini Mungu aliwafanya kusimama kimya na kuangalia Utukufu wa Mungu kufumbua macho, na upofu, mambo kwa watu wanaoteseka.

102 Huko Karlsruhe, Ujerumani, alasiri moja wakati mwanamizimu alipojitokeza, ili. . . walitaka kubishana nami, pale hotelini. Yule mtu asingewaruhusu waingie. Wakasema, "Tutatupa uchawi kwenye mkutano huo alasiri ya leo na hakutakuwa na mtu yeyote atakayekuja. . . " Hapana, alisema, "Tutailipua, kwa dhoruba." Nayo anga ilikuwa nzuri tu na angavu. Lakini tulipofika pale na kuanza tu kuimba, dhoruba kubwa sana ikatokea. Kulikuwa na kama ishirini upande wangu mmoja, na ishirini upande huo mwingine. Na wote walikuwa wakipitia uganga wao na kukata manyoya yao kwa makasi, na

kupitia mambo kama hayo, kutupa uchawi. Ndipo, kwa ghafula, hiyo hema kuu inayoenea elfu thelathini ikaanza kutetemeka na kutikisika, huku pepo zikivuma. Nami nilikuwa nikihubiri. Ndipo Kitu fulani kikasema, “Simama kimya.”

103 *Haleluya!* Sisemi samahani. Hiyo inamaanisha, “Mungu wetu asifiwe!”

104 Naye Mungu akaifanya dhoruba hiyo kusimama kimya, ikarudi nyuma, ili kuona sifa za Mungu, ambapo karibu watu elfu arobaini, mchana na usiku huo, waliingia katika Ufalme wa Mungu, kwa njia hiyo. “Simama kimya.” Hiyo ni kweli. Yeye hutoa ushahidi.

105 Huko Uswidi au Uswisi . . . Vema, hapa, nitasema, kule Ufini, siku moja, mvulana mdogo aliyekufa alikuwa amelala kando ya barabara, gari lilikuwa limemkanyaga, likauponda mwili wake vipande vipande. Alikuwa amevunjika sana hata mguu wake ukachomoza kwenye soksi yake. Gari lilimgonga na kumkanyaga, kama kitambaa namna hiyo, kisha likamrusha hewani na kumtupa kando ya barabara. Macho yake yalikuwa yametokeza nje. Kinywa chake kilikuwa wazi. Ulimi wake ulikuwa ukining’inia na damu ikitoka masikioni mwake. Lakini, miaka miwili kabla ya hapo, Mungu alikuwa ameonyesha ono lake. Nami nilikuwa nimetembea kijinga sana, na kumtazama huyo mtoto; nikaondoka, nikilia.

106 Naye Bwana, ama mtu fulani, kimbinguni, akaweka mikono yake begani mwangu. Kasema, “Huyo si ndiye yule mvulana niliyekuonyesha?” Loo, ni hisia ya jinsi gani!

107 Hapo alisimama Meya wa mji, Mtu Mashuhuri, anavyoitwa, na wengi wamesimama karibu. Naye Mungu akawafanya kusimama kimya, apate kuonyesha Nguvu Zake kuu za kumfufua mfu, ampe uhai tena. “Simama kimya.” Mwamini Mungu, na uwe shahidi. Neno Lake ni la Milele.

108 Ilikuwa siku chache zilizopita, tulipokuwa . . . Ili tu kuona jinsi Mungu anavyofanya mambo rahisi sana! Nasi tumechanganyikiwa sana, mpaka tunatazamia mambo makubwa sana. Tosheka na mambo madogo. Mwangalie anapofanya kazi Zake tukufu, jinsi anavyokulinda. Usiwe ukiangalia mbali sana juu ya kitu fulani; angalia hapa chini.

109 Angalieni. Nikaanza kuwaza hivi, kwamba inawezekana mtu, kama wale mitume, na wakati unapoweza kuishi karibu na Mungu; na Mungu, kwa neema Yake, anatenda kazi kupitia kwako; kwamba kadiri unavyozidi kumpata Mungu, ndivyo unavyozidi kuwa mtauwa. Kadiri Uzima wa Milele unavyoingia, ndivyo unavyozidi kusukumia nje mambo ya kiakili.

110 Sasa, simaanishi kuwa mlokole. Ninamaanisha kuwa mwaminio halisi, mwenye akili timamu, imara. Mnaona? Si kundi la itikadi, bali mwaminio thabiti, wa kweli, mwenye busara, mwenye akili timamu.

111 Na sasa tazameni. Nimeona ikifanya kazi. Na kufikiri ya kwamba kama utaingia katika mawasiliano hayo na Mungu, inakuwa hata si sauti yako tena. Sio wazo lako tena. Inakuwa wazo la Mungu na Sauti ya Mungu. Wewe ni mzabibu tu, ama, tawi tu, Yeye ni Mzabibu, na ni Roho Wake ndiye aingiaye na kutia nguvu. Maadamu unaweza kujiondoa njiani, Yeye ataijaza, na ndipo unaweza kuwa shahidi.

Kama vile tu safina ya Nuhu ilivyokuwa shahidi.

112 Kama vile Yesu alivyokuwa shahidi wa Mungu. Alijazwa sana na Mungu hata Yeye na Mungu walikuwa mmoja. "Mungu alikaa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake," Usemi wenyewe. Matendo ya mtu hutangaza tabia yake, Kristo alikuwa kazi ya Mungu, naye Kristo alitangaza tabia ya Mungu: hisia Zake kwa wagonjwa, hamu Yake ya kuwaokoa watu, mpaka hata akautoa uhai Wake Mwenyewe. Kazi ya Mungu . . . Tabia ya Mungu ilitangazwa katika Kristo.

113 Na kama unaweza tu kuondoa mawazo yako mwenyewe ya kiakili, na kumpa Mungu nafasi, anaweza kutangaza tabia Yake kupitia hiyo kazi ya kujitoa kwako. Jifanye tupu. Ondosha ulimwengu, ondoa mashaka yako, njiani. Ikiwa umekuja madhabahuni kuombewa, useme, "Nitapanda nione kama nitapona," Mungu kamwe hawezi kutangaza kazi Zake. Huna budi kuyaondoa mawazo yako mwenyewe, na umruhusu Yeye akujaze.

114 Sasa, jinsi ninavyoona mambo haya; kama vile maskini fahali huyu alivyotaka kuniua wakati huo; kama wale mavu huko nyuma kwenye ua; kama mambo mengine mengi ambayo yametendeka; dubu msituni. Ni uchunguzi wa maumbile. Ni kitu kinachotokea.

115 Ninasema hili sasa, samahani, kama uzoefu wa kibinafsi, lakini nataka kuwaambia kwa sababu ni wakati wa kisasa. Mtu fulani alisema, "Loo, vema, mambo hayo yalitukia huko nyuma katika siku za manabii. Katika siku . . . " Naam, Mungu alikuwa anaonyesha mifano. Lakini je, ulijua, siku hizi, Mungu anajenga Kanisa? Unasema, "Vema, Yeye alikuwa na manabii. Iliwabidi kunena Neno la Mungu." Lakini, Yeye ana Kanisa la Mungu, leo.

116 Angalia, kuna jambo linatukia. Laiti ingaliweza kuwa wakati wote. Natamani kwa Mungu kwamba ingeweza kuwa wakati wote, lakini sivyo. Inakuja tu kwa mapenzi Yake.

117 Sasa, siku chache zilizopita, ama yapata majuma mawili ama matatu yaliyopita, nilikuwa nikiwaombea watu wenye lukemia. Nilikuwa nikiomba pamoja na watu, nikingojea ono, ambao ni wagonjwa na wanaoteseka. Wengi nimengojea, kwa miaka.

118 Kwa mfano, maskini Edith Wright, mlemavu. Ninakumbuka wakati baba yake alipokuwa amelala, akifa, naye Mungu akaonyesha ono kwa ajili ya baba yake, na kumwacha Edith alale hapo.

119 Kuna msichana, na—nadhani bado yuko hapa ndani. Bibi Geiger, kutoka Fort Wayne, maskini mama mwenye sura ya huzuni, msichana. Alijifungua mtoto. Naye huyo mtoto alikuwa mkubwa sana; yeye alikuwa mdogo sana, ikamwambukiza kansa. Naye Mungu akamponya hiyo kansa. Sasa nusura arukwe na akili, kutokana na wasiwasi. Yuko kwenye kukoma kwa hedhi. Basi maskini mwanamke huyo. . .Na mume mwaminifu kweli. Na maskini jamaa huyo ameenda kila mahali, akiomba, na kutafuta, na kulia. Nami nikiwaombea watu kama hao.

120 Nanyi mnajua nini kilichotokea? Ndugu Wood kule nyuma, baba yake alishuka, Shahidi wa Yehova. Ndugu Wood alikuwa Shahidi wa Yehova. Mungu alishuhudia na kujitangaza Mwenyewe kwake, kwa kumponya mvulana wake, David, kiwete.

121 Kisha ndugu yake akashuka. Naye ndugu yake alikuwa akiishi maisha machafu. Na hapo Roho Mtakatifu akageuka na kumkemea. Kamwona mwanamke aliyekuwa akikimbia naye, naye akayasalimisha maisha yake na kumwacha kila ibilisi amtoke siku hiyo. Naye anatembea mitaani sasa akifanya kila awezalo kumtumikia Mungu, akiwashuhudia watu wake.

122 Halafu, maskini babake mzee, mwaminifu jinsi angeweza kuwa, katika shughuli zake zote kama mkulima, na kadhalika. Basi wakati baba yake aliposhuka, alitaka niende kuvua samaki pamoja naye, nasi tukashuka ziwani.

123 Tukienda zetu njiani, ono likaja, asubuhi hiyo. Naye akasema, "Kila ziwa mtakalovuka na kila mkondo wa maji, litakuwa na matope; hakuna uvuvi. Lakini mtakapofika chini kwenye kile Kijito cha Mbwa Mwitu kule, kwenye Bonde Wazi," kasema, "hayo yatakuwa mazuri na ya bluu. Wala hujawahi kumshika kambare kwenye maji hayo, lakini utashika msururu mzima wao. Na," kasema, "watamshika mmoja mdogo au wawili wadogo. Na kisha utamshika samaki mkubwa, pamoja na samaki wa magamba. Atakuwa wa spishi, kubwa."

124 Niligeuka na kuwanukulia. Nikatazama macho ya yule mzee, huku akiwatazama wavulana wake. Tuliposhuka pale na kuingia ndani ya maji. . .Kila ziwa lilikuwa na matope, tukishuka. Tulipofika pale, yalikuwa ni bluu tu, karibu yangeyaumiza macho yako. Nasi tukavua samaki, wala hatukuweza kupata besi, krapie, au chochote. Ndipo, mara ghafula, nikaanza kushika kambare, na nikashika msururu mzima wao. Baadhi yao, pauni tano, kila moja. Na wakati mwingine wawili kwenye mstari mmoja, kwa ufito na ugwe wa kuvulia. Tulivua samaki, tukapata msururu wa samaki.

125 Ndipo kesho yake asubuhi, nikarudi, nikivua samaki. Nikamkamata mmoja mkubwa mwenye shavu la bluu, ilikuwa. . .au kile tunachoita samaki mwenye tumbo nyekundu, mkubwa sana niliyepata kumwona.

126 Basi, mtu huyo alipokuja kwangu, nilisema, "Sasa, bwana, Biblia ilisema, 'Akiwepo miongoni mwenu mtu wa kiroho, na nabii, na yale anayosema yanatimia, basi msikieni. Yasipotimia . . .'" Nami nilichukua matabiri manne mashuhuri sana ya Mashahidi wa Yehova na kumwonyesha kwamba hakuna hata mojawapo ambalo lilikuwa limetimia; kila moja halikutimia. Nikasema, "Sasa vipi kuhusu hao samaki?"

127 Naye Mungu akaonyesha ono hilo, kumbadilisha huyo mtu na kumgeuza, kwa ajili ya mtu huyo mmoja, ambapo kulikuwa na maelfu wamelala, wakiteseka. Ni ukuu wa Mwenyezi Mungu, kukujulisha kwamba Yeye hutangaza matendo Yake kwa kazi Yake, na tabia Yake inatangazwa kwa njia iyo hiyo.

128 Tazama lile birika la Bethesda. Unasema, "Hiyo haisikiki kama Mungu akifanya hivyo." Waangalie vilema, viwete, waliopindika, vipofu, waliopooza, wanaongoja. Naye huyu hapa Yesu anakuja moja kwa moja kupitia pale, mavazi yaliyojaa nguvu; ndipo akamwendea mtu mmoja, na kumwendea mtu ambaye angeweza kutembea, kufanya chochote alichotaka, lakini alikuwa na aina fulani ya ugonjwa uliodumaa. Naye akamponya, na kuwaacha wengine wao wamesimama pale. Mnaona? Tabia Yake. Alitaka kuonyesha Nguvu Zake. Alitaka kufanya jambo fulani. Naam, ulimwengu unasimama kimya, kuliona.

129 Sasa angalieni, hivi majuzi, tuliporudi. Nilirudi, ule mkutano wa Indianapolis, nami nikawazia ingenibidi kukaa kwa muda kidogo tu, mbali na watu, mpaka kwa namna fulani nipumzike, maana ningekuwa na saa ishirini ama thelathini, kwa siku, kwenye mahojiano ya faragha, na maono hayo yakija. Nilikuwa karibu na kufa nilipofika nyumbani. Hakuna anayejua ninachopitia juu ya hayo; hakuna mtu. Hakuna njia ya kulielezea. Lakini basi mimi, Ndugu Wood, na ndugu yake, tulikimbia kwenda mahali pale, na kuvua samaki tena, mchana na usiku.

130 Ndipo alasiri hiyo, tukiwa tumeketi huko nyuma, Ndugu Wood alianza kuzungumza juu ya mwanamke mkongwe aliyekuwa mfuasi wa Anderson church of God, hapa juu, walipokuwa katika upeo wa ujana wao. "Ni vizuri jinsi gani!" Alisema jinsi alivyokuwa akiwachukua wavulana hao wadogo wa Mashahidi wa Yehova na kuwapenda. Ndipo Ndugu Wood akamwambia ndugu yake, Lyle; akasema, "Lyle, si lingekuwa jambo zuri sasa, kama tungeenda kumtafuta dada huyo mkongwe na kumjulisha kwamba tumeokoka?"

131 Sasa, neno hilo lilipata kibali kwa Mungu. Baada ya kuzungumza juu ya Mungu kwa muda mrefu sana, lakini neno hilo lilipata kibali. Hao wavulana wawili Mashahidi wa Yehova, wote wawili wakiwa watu wazima, wakitaka kumtafuta

mwanamke mkongwe na kumwambia kuwa wameokoka, ndugu wawili.

132 Waliposema hivyo, Roho wa Mungu na ukuu Wake ulinishukia, nikiwa nimeketi pale kwenye mashua hiyo. Loo, laiti ningalikuwa na sauti, kwa njia fulani, na ningeweza kulizamisha hilo mioyoni mwa watu. Nisingeweza kujizuia zaidi ya vile ungeweza kuruka hadi mwezini; kwa neno hilo tu. Nami nikasema, "Jamani, kuna jambo linakaribia kutukia. Ni mnyama mdogo wa aina fulani. Atafufuliwa. Kutakuwa na uhai ulioambatanishwa nalo. Na mtaliona mara moja."

133 Nami nikawazia, "Sasa nimesema nini?" Nami nikaanza kufikiria mambo kadhaa. "Ni nini kilinifanya niseme hivyo?" Hakuna ono. Ilikuwa ni kitu Fulani tu kilichozungumza. Ilikuwa ni nini? Haikuwa akili zangu; nisingeweza hata kuwazia jambo kama hilo. Ilikuwa chini ya hapo. Ilikuwa ni kwenye moyo ambapo Mungu alikuwa ameingia. Alikuwa anazungumza. Sikuninii, hata sikuwazia jambo kama hilo, Naye akanena.

134 Nadhani hapo ndipo Yesu aliposema, "Ukiamini moyoni mwako, na utauambia mti huu, au mlima huu. Wala usiwe na shaka, bali uamini kwamba kile unachosema kitatokea, kitakuwa chako."

135 Hiyo hapo hoja yangu. Fikia mahali hapo, mahali ambapo ni kitu Fulani ambacho si wewe mwenyewe. Ni Kitu fulani zaidi ya mawazo yako, kinachozungumza.

136 Tuliendelea. Kwa kumalizia, nasema hivi, Ndugu Wood na hao wengine wameketi hapa kama mashahidi, kesho yake asubuhi . . .

137 Usiku huo, tulienda, na Bwana akatupa usiku mzuri wa kuvua samaki. Hakuna aliyeshika samaki . . . Nasi tukawashika watatu pale, katika dakika chache tu, na hao watatu walikuwa na uzito wa karibu pauni ishirini. Nasi tulikuwa na msururu mkuwa wa samaki.

138 Kesho yake asubuhi, tulirudi na kuweka vyambo, vipya, kwenye ugwe wa kuvulia, wala hamna samaki hata mmoja. Walikuwa wamekwisha. Nikasema, "Hebu tuingie kwenye ghuba hili dogo na kupumzika kwa dakika chache, ndugu. Nasi tutavua samaki wenye shavu la bluu, kwa ugwe wa kuvulia."

139 Tukarudi kule na tulikuwa tukivua samaki wenye shavu la bluu, kule nyuma kwenye lile ghuba dogo, na mashua yetu. Na kila wakati, tulisimama tu muda wa kutosha, mota ingesimama. Hatukuwa tukivua; tulikuwa tunazungumza juu ya Mungu.

140 Naye Bw. Lyle, ambaye sasa ni . . . Alimwendea dada yake, akajaribu kumtoa kwa Shahidi wa Yehova. Naye akamwambia, yeye—yeye akamwambia alikuwa akisikiliza mashetani; kwamba tulikuwa mashetani.

141 Kasema, "Lyle, unajua vyema kuliko hivyo. Na mambo haya yote fulani."

142 Ndipo, Lyle akashika samaki mdogo mwenye shavu la bluu, karibu *hivyo*. Naye alikuwa akizungumza, kwa hiyo alimwacha maskini jamaa huyo mdogo ameze hiyo ndoano kubwa. Ikaenda moja kwa moja hadi tumboni mwa huyo samaki mdogo. Na alipoishika, hakuweza kuivuta. Kwa hiyo akamfinya tu mkononi mwake, akaifunga na kumtoa matumbo. Ilimbidi kutoa ndoano hii kutoka kinywani, kwa maana kama angeikata ndoano hiyo, ingeninii. . .samaki aliyekufa, atakufa kwa vyovyote vile. Basi haya hapa maneno aliyosema, "Hakika umefika mwisho wako, jamaa mdogo," na kumtupa majini.

143 Naye akaruka mara tatu ama nne, kisha akaenda akizunguka kwenye hayo maji ya bluu, mpaka akafika chini. Akalala hapo kwa dakika chache tu. Kisha akarudi juu, juu ya maji, na kupapatika mara tatu ama nne. Mapezi yake madogo yakanyooka, namna *hiyo*, akalala kwa upande mmoja, amepindika. Na kwa yapata dakika ishirini, sisi tukivua samaki, alikuwa amekwisha kuelea kuingia nyikani tena, nyuma kwenye takataka fulani. Nami. . .

144 Ndipo mtu fulani akasema, "Hao samaki wadogo kweli wanakula kiamsha kinywa, wanakula."

Nikasema, "Naam. Hiyo ni kweli."

145 Nasi tukasema, "Loo, Mungu si ni mkuu!" Naye Ndugu Wood akasema, "Loo, ni jambo zuri sana, Ndugu Branham! Tunayo fursa ya kuwa hapa pamoja nawe." [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

146 "Loo," nikasema, "usifikiri hivyo, Ndugu Wood. Huu," nikasema, "sio m—mlima mtakatifu. Sio mahali patakatifu. Ni Mungu mtakatifu. Si mtu mtakatifu, bali Mungu mtakatifu." [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

147 Basi tulipokuwa tukizungumza, Kitu fulani kilinigusa. Kasema, "Nitaonyesha Nguvu Zangu sasa." Kabla sijajua nilichokuwa nikizungumzia, Maandiko hayo yakanijia akilini mwangu, "Lolote usemalo, amini ya kwamba litatokea, moyoni mwako. Sema, nayo yatakuwa yako." Ka—karibu naweza. . . Yalikuwa yakibubujika kutoka kwangu.

Nami nikawazia, "Ni nini hiki kinaendelea?"

148 Lyle na Banks wameketi pale. Tulikuwa tunavua samaki. Yule samaki mdogo aliyekufa amelala, kama dakika ishirini, amejikunja kabisa pale, akaelea tena mahali pale; matumbo yake madogo yakining'inia kutoka kinywani mwake. Nami nikamwangalia yule samaki mdogo, ndipo wazo likanijia, "Akawaambia hao wavuvi, 'Twekeni upande wa pili wa mashua.' Wakaliamini Neno Lake. Petro akasema, 'Bwana, tumevua

samaki usiku kucha, wala hatujapata chochote. Hata hivyo, kwa Neno Lako, tutatupa wavu.'" Hilo hapo, "Kwa Neno!"

149 Kitu fulani kikaniambia, "Mungu anawajua samaki. Nena tu Neno nawe utaona kitakachompata samaki huyo."

150 Nikasema, "Ewe samaki mdogo, katika Jina la Yesu Kristo, fufuka."

151 Naye Mungu, hakimu wangu mkuu, pamoja na hao watu wawili wamesimama pale, samaki huyo mdogo akageuka ubavuni mwake na kuogelea akaondoka pale upesi alivyoweza kwenda, akiwa hai tena. "Nena Neno!" Mwenyezi Mungu, ninaposimama hapa mbele Zake mbele ya kundi hili na Biblia hii, anajua hiyo ni kweli.

152 Wakati watu wanakufa, na hata hivyo Mungu alionyesha Nguvu Zake kwa wale Ma-. . .Mashahidi wawili wa Yehova, ya kwamba Yeye ndiye ufufuo na Uzima, na hakuna kitu ila yale anayojua Yeye. "Unasema, na kuamini kwamba kile unachosema kinatimia, kitakuwa chako."

153 Ilikuwa ni nini? Mungu akionyesha Nguvu Zake; si mimi, mzabibu tu. . .au tawi. Alitia nguvu hilo tawi ili nisiweze kujizuia kutoa sauti hizo. Ningewezaje kufikiria juu ya samaki mdogo, aliyekufa amelala pale, wakati hata tuliwakata na kuwaweka kama chambo kwenye ugwe? Huyo samaki mdogo akining'inia pale, amelala pale, amekufa.

154 Bw. Wood na hao wanaoketi papa hapa, wakinitazama sasa, shahidi wa jambo hilo. Ndipo Roho wa Mungu akashuka kupitia bonde hilo, mpaka ungefikiri Unyakuo ulikuwa unakuja. Hata, mpaka, Bw. Wood akapaza sauti na kusema, "Loo, ni vizuri kuwa hapa!" Kasema, "Ndugu Branham, tuna furaha sana kuwa hapa!" Tamshi pekee walililoweza kunitolea lilikuwa ni mimi kuwa ndugu yao. Nami nikageuka haraka. . .Maana, waliona ya kwamba Mungu alikuwa amenitumia kunena uhai kwa samaki.

155 Na, sasa, hilo linasikika kuwa la kichaa, lakini huyo ni Mungu yeye yule aliyenena uhai kwa yule oposamu aliyekufa akiwa amelala kule uani. Yeye ni Alfa na Omega, Mwanzo na Mwisho. Yeye ndiye Uzima, ufufuo. Yeye ni Uweza, Yule wa milele. Yeye yule jana, leo, na hata milele!

156 Hilo linanipa kujua hili, ya kwamba siku moja, wakati uhai umetoka kwenye mwili huu upatikanao na mauti, nami nimelala kule, hata hivyo, kama anajali samaki, hakika Yeye ananijali mimi na wewe, ambao tunajaribu kumtumikia. Na siku moja tukufu Yeye atakuja. Si tawi, bali Mzabibu Wenyewe utanena kutoka makao makuu Yake Utukufuni, na wale waliolala katika Kristo watafufuka na kwenda kwenye Uzima wa milele.

157 Ni hisia iliyoje! Hakuna aliyeweza kuielezea. Ukimwona samaki aliyekufa amelala juu ya maji, na matumbo yake yamevutwa kupitia kinywa chake, na mtu mwenye mikono

mikubwa ambaye alimbinya huyo samaki, *hivi*, na kumchukua na kumwangamiza. Na ungeweza kumsikia akichanika, aliporarua matumbo kutoka kwa huyo samaki. Akamtupa jamaa huyo mdogo majini. Alitetemeka mara nne ama tano, akaacha, wala hakuna lingine. Kumwona maskini jamaa huyo, katika dakika moja tu ya kunena Neno hilo, [Ndugu Branham anadata vidole vyake—Mh.] akarudi katika hali yake, akiwa hai tu kama alivyowahi kuwa, na kuogelea kupitia maji hayo, haraka tu kama alivyoweza kwenda, akirudi nje kuungana na samaki wenzake.

158 Yeye ni Mungu. Alijua samaki huyo alikuwa pale. Vile vile tu Yeye alijua ya kwamba mmoja alikuwa na sarafu kinywani mwake. Vile vile tu alivyojua kama angetupa . . . Ikiwa watu hao, wanasema . . . Katika Marko Mtakatifu mlango wa 5, ilisema ya kwamba Yesu aliazima mashua ya Petro pale na kwenda kuvua samaki. Sasa, alisema, "Tweka hadi kilindini mkavue samaki." Wakati walipokuwa wamevua samaki, wakati . . . Hata walijua walikuwa wamevua samaki usiku kucha wala hawakupata chochote. Kama vile tulivyokuwa tumefanya jambo lile lile, wala hatukushika chochote. Lakini, Mungu alitaka kuona kama wangeliamini Neno Lake, kwa hiyo akasema, "Tweka hadi kilindini, mkavue samaki." Kama hapakuwa na samaki pale, kuliamini Neno la Mungu kutaweka wengine pale. Hamna lingine kwake.

159 Kisha, Mungu yeye yule, katika tabia Yake ile ile iliyokuwa hapo mwanzo, ni Mungu yeye yule kwa tabia iyo hiyo leo. Yeye ni wa Kwanza, wa Mwisho. Ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Yeye angali ni Mungu.

160 Kwa hiyo, ninyi mlio hapa asubuhi ya leo, na kuombewa, hebu niwaambie jambo fulani. Kuona shuhuda hizi, na Mungu ni shahidi kama ni za kweli au la, hiyo ni kweli, mnatafuta mambo makubwa. Mnajaribu kuangalia jambo fulani kubwa hapa, wakati liko papo hapo karibu nanyi. Hiyo ni kweli. Mungu yeye yule aliyeweka njaa nafsini mwako, kuja kuombewa, ni Mungu yeye yule aliyempa samaki huyo uhai; Mungu yeye yule aliyemzuia yule fahali shambani; Mungu yeye yule aliyemwua yule mwendawazimu pale mbele yangu; Mungu yeye yule aliyemtoa Danieli katika tundu la simba; Mungu yeye yule aliyesema, "Tupeni nyavu zenu upande huu mwingine, mkavue samaki." Ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

161 Kazi Zake haziwezi kushindwa. Tabia Yake haiwezi kushindwa. Na matendo Yake yanatangaza tabia Yake, kwa hiyo amefufuka leo na yuko hapa katikati yetu, yeye yule jana, leo, na hata milele. Nasi ni mashahidi wa tabia Yake.

162 Tabia Yake imenibadilisha. Iliponijia, wakati mmoja nilikuwa mwenye dhambi; na sasa nimeokoka. Wakati mmoja nilikuwa nimepotea; sasa nimepatikana. Wakati

mmoja nilipenda mambo ya ulimwengu; nayachukia sasa. Wakati mmoja sikumjali Mungu; ninampenda sasa. Kitu fulani kilinitokea. Kitu fulani kilikutokea. Ni nini? Ni kazi ya Mungu ikitangaza tabia Yake.

163 Anatupenda. Anajali masilahi yako. Anajali uponyaji wako. Anaijali roho yako. Je, hutamruhusu awe na njia Yake maishani mwako? Usimtilie shaka bure. Nenda zako, ukimwamini, na Mungu atakupa shauku ya moyo wako, kwa kuwa ni mapenzi Yake mema kufanya jambo hilo. Anatamani kulifanya. Lakini, jambo ni kwamba, sote tunafadhaika. Simameni kimya!

164 Angalia, useme, "Mungu, hiyo inamaanisha mimi. Haijalishi ni nani anayeniombea, ni nini kinachoniombea." Haihitaji Oral Roberts, Billy Graham, au William Branham, au A. A. Allen. Inahitaji Mungu. Hiyo ni kweli. Inahitaji imani yako, iliyotiwa nanga huko katika Mungu.

165 Useme, "Mungu, ni Kweli, na hapo pekee ninasimama." Na hebu hilo libaki humu *ndani*, mpaka lishuke liingie *hapa,* kutoka kichwani mwako hadi moyoni mwako, kuwa . . . na kuwa uhalisi, ndipo itafanya kazi. Inaweza tu kufanya kazi inapokuja moyoni.

166 Bwana awabariki sasa, tunapoinamisha vichwa vyetu. Weka shauku yako moyoni mwako. Iweke mbele za Mungu, sasa hivi, (Je, utafanya hivyo?) tunapoomba. Ikiwa ni kwa ajili ya wokovu, ikiwa ni kwa ajili ya . . . Vyovyote ilivyo, iweke mbele za Mungu sasa hivi tunapoomba.

Imani yangu inakutazamia Wewe,
Ewe Mwana-kondoo wa Kalvari,
Mwokozi wa Kiungu;
Sasa nisikie ninapoomba,
Ondoa hatia yangu yote,
Loo nijalie tangu leo
Kuwa Wako kabisa!

Ninapopitia kwenye mzingile mweusi wa maisha

Iweni kimya sasa.

Na huzuni ikinizunguka,
Kuwa Kiongozi wangu;
Amuru giza liwe mchana
Futa hofu zangu zote,
Wala usiniache nipotee
Kutoka Kwako kwenda kando.

167 Bwana mbarikiwa, tungeweza kusema kama wale waliosimama juu ya mlima siku ile, na kusema, "Ni vizuri sisi kuwa hapa. Nasi tungejenga vibanda vitatu, tuweke wachungaji katika kila kimoja." Lakini ile Sauti ikageuka haraka na kusema, "Msikieni Yeye. Yeye ni Mwanangu." Sasa na tuwaache wachungaji, kutoka akina Musa na akina Eliya,

na kutoka watu mashuhuri wa dunia, ingawa tunashukuru kwa ajili ya wote. Lakini, ulisema sisi tumsikie Yeye.

168 Nalo Neno Lake lilisema hivi, (si neno la mchungaji, wala la mwinjilisti), "Yoyote mtakayo, mkiomba, aminini ya kwamba mnayapokea, yatakuwa yenu. Ukiuambia mlima huu, 'Ng'oka, ukatupwe baharini,' wala usione shaka moyoni mwako, bali uamini ya kwamba hayo uyasemayo yatatimia, yatakuwa yako." Si lazima itokee mara moja, wala haikutokea mara moja kwa Ibrahimu na Sara.

169 Lakini ulisema, "Ukiamini kwamba unayosema yatatukia, yatakuwa yako." Sasa, Baba, haya hapa maombi yetu. Tuchukue sasa hivi. Ichukue mioyo yetu mikononi Mwako na uibinye sana kwa upendo, ukisukuma woga wote na kutokuamini kutoka kwao, kuwafanya kuwa wazi na watupu. Na kisha uwajaze mara moja na Roho Wako, kama ile lami na bereu zilivyoingia ndani ya safina, kuzuia hofu na mashaka yasije tena mioyoni mwetu. Na utufanye kazi Yako, ili uidhihirishe tabia Yako, kwa ulimwengu, kupitia kwetu, kama nyaraka zilizoandikwa zinazosomwa na watu wote.

170 Jalia kila mmoja aliyekuwa. . . waliotiwa mafuta, hivyo ndivyo ulivyosema wafanye, jalia wapate kuponywa, leo, kuanzia, kila mtu, kuanzia maumivu ya meno ya kawaida, hadi vipofu, wanaoteseka, ama chochote kile, imani hiyo na ikolee sasa katika huo moyo uliokuwa na hofu na mashaka ulipoingia.

171 Na, Ee Mungu, daima ninakumbuka . . . Mimi mwenyewe, sisi watu watatu; kama vile Petro, Yakobo na Yohana waliposimama kwenye Mlima wa Kugeuka Sura na kuona ulichofanya kule. Hatutawahi kusahau maskini lile ghuba dogo huko Fanny Creek, mradi tu tuna kumbukumbu na kukumbuka. Huenda isiwe na maana kubwa kwa ulimwengu, lakini tulipoona nguvu kuu za Mungu, uwepo wa kila mahali wa Mungu aliye hai ukishuka na kuwa na huruma, ya kutosha juu ya wanadamu, kuonyesha Nguvu Zako, kwa kumrudisha yule samaki mdogo aliyekuwa amekufa juu ya maji, kuwa hai tena, hilo linaruka moja kwa moja juu ya mtu mkosoaji au asiyeamini. Lakini, jinsi linavyoshikilia katika moyo wa Kikristo!

172 Tunajua ya kwamba Wewe ndiwe Mungu. Wewe ni Mungu yeye yule hapa katika chumba hiki asubuhi ya leo. Ni zaidi sana vipi unawajali watu katika chumba hiki, wanaume kwa wanawake, kama unavyomjali samaki mdogo! Huyo samaki mdogo alimaanisha nini Kwako? Hakuna kitu; kutangaza tu matendo Yako. Nami naomba, Mungu, ya kwamba utatangaza matendo Yako katika kila mwanamume na mwanamke, mvulana na msichana, hapa ndani leo.

173 Ikiwa kuna wengine hapa, Bwana, wasiokujua Wewe, kama Mwokozi wao, bado hawajapata tukio, nao wangetaka kuimwaga mioyo yao, leo, kutoka katika mambo yote na

takataka za ulimwengu, ili uwajaze upendo mioyoni mwao, kama Nuhu alivyoifanya safina kwa lami, ninaomba ya kwamba utakuwa pamoja nao, katika dakika hizi za muda mfupi sasa ambazo zimesalia kwenye ratiba. Tujalie, Baba, kupitia Jina la Yesu.

Na wakati vichwa vyetu vimeinamishwa:

> Neema Yako tele inijalie
> Nguvu kwa moyo wangu unaozimia,
> Ivuvie bidii yangu;

174 Sasa, kama unamtaka Kristo, wakati wanaimba, unataka kuumwaga moyo wako, asubuhi ya leo, na Mungu akuchukue jinsi tu ulivyo hapo, waweza kumwinulia mkono wako? Sema, "Nikumbuke." Mungu akubariki, bwana. Na wewe, bwana. Wewe, dada. Wewe, ndugu. Wewe. Mtu mwingine, mkono wangu wa kulia? Inua mkono wako. Mungu akubariki, dada. Mtu mwingine aseme, "Ninataka kufanya tupu moyo wangu." Mungu akubariki, dada, huko nyuma.

> Nijalie tangu siku hii
> Kuwa Wako kabisa!

175 Mtu mwingine anataka kuinua mkono wake sasa, kabla tu ya maombi?

176 Mungu Baba, umeona kila mkono. Saba au minane, mikono kumi iliinuliwa. Sasa wanaondoa hofu zao zote na kutoamini. Sasa wanakudai Wewe kama Mwenye kuwatosha kwa yote, kama Mpenzi wao, kama Mwokozi wao, kama Mponyaji wao. Mashaka na hofu zote, wanatamani kuondolewa kutoka kwao. Ninaomba ya kwamba utanijalia, Bwana, kwa neema Yako kuu. Na itokee leo tu.

177 Wewe ambaye ungeweza kunena uhai kwa samaki; kunena uhai kwa mvulana mdogo aliyekufa; ukanena uhai kwa Elij' Perry aliyelala pale, amekufa, na mikono yake imekunjwa; ukanena uhai kwa mtoto mchanga, aliyekufa kule Mexico; ukanena uhai huko katika Lazaro, baada ya kufa siku nne, ni zaidi sana jinsi gani tunaweza kuchukua msimamo wetu, leo, juu ya Mwamba wa Neno Lake la Milele, na kutazama ng'ambo ya kivuli hiki cha shaka, kwake Yeye aliyesema, "Mimi ndimi ufufuo na Uzima." Imani yangu na ipate mahali pake pa kutulia sasa juu Yake, ule Mwamba imara, Kristo. Na jalia wapokee kila kitu ambacho wameomba. Sikiliza maombi yetu tunapoomba katika Jina la Kristo. Amina.

> Nampenda, nampenda
> Kwani alinipenda kwanza
> Na kununua wokovu wangu
> Mtini Kalvari.

178 Sasa tunapoimba tena, peana mikono na mtu aliye karibu nawe. Tulia tu sasa, tuna . . . Ibada bado haijaisha, mnaona.

Nampenda,

. . .?. . .

Kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

179 Je, unahisi kusuguliwa kabisa? Unajisikia bora sasa? Unajisikia kama . . .? Neno! Ni—ni—ni—ni Damu ya Bwana Yesu itakasayo, ambayo huenda moja kwa moja moyoni, hutusafisha na dhambi na uovu wote.

Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

Sasa, Ndugu Neville.

57-0623 Amini Kutoka Moyoni
Branham Tabernacle
Jeffersonville, Indiana Marekani

SWAHILI

©2023 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org